

# Nimerudi Okombe

Meandika kwa huzuni, Wakenya twaomboleza,  
Machungu kwetu moyoni, mesalia kwenye giza,  
Okombe wetu jamani, tumeshindwa jituliza,  
Kwaheri Mike Okombe, shujaa wetu imara.

Ujumbe tulipokea, tukakosa kuamini,  
Wakenya kuulizia, kokote mitandaoni,  
Wakitaka kuyajua, metokea na kwa nini,  
Kwaheri Mike Okombe, shujaa wetu imara.

Duniani lisifika, raga ukituchezea,  
Uwanjani ukafika, tuzo ukatuletea,  
Mataji walikuvika, Kenya wakatusifia,  
Kwaheri Mike Okombe, shujaa wetu imara.

Familia mepoteza, timu yako mepoteza,  
Kocha wako mepoteza, wachezaji mepoteza,  
Kenya yetu mepoteza, ulimwengu mepoteza,  
Kwaheri Mike Okombe, shujaa wetu imara.

*SEME DUNCAN  
‘Malenga wa Kiminini’  
Chuo Kikuu cha Seku*